2020 FORM 4 TERM 1 ENTRY EXAMS

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

SEHEMU A: USHAIRI (LAZIMA)

USHAIRI

1.a. - Ni shairi huru kwa sababu mshairi ametumia (i) mishata mf. katu, eti, niondoke

- Shairi lina umbo la paa la nyumba

- Matumizi ya alama za uakifishaji kwa wingi (al. 2)

b. (i) Anatishwa kwa risasi

(ii) Kupigwa mateke na mikuki

(iii) Kuponda mali yake

(iv) Kuletewa hatimiliki bandia *(mwalimu akubali hoja nyingine yoyote)* Al. 4

c. (i) Huzuni

(ii) Ujasiri (2 x 1)

(iii) Uchungu

d. Shairi lina beti saba

Kila ubeti una mishororo sita

Lina umbo la paa la nyumba (3 x 1)

e. Usambamba – Ni urudiaji wa kiwango cha sentensi, kirai (n.k)

mf. (i) Niondoke, mimi niondoke hapa, niondoke hapa kwangu

(ii) Siondoki, siondoki, siondoki niondoke hapa kwangu (2 x 1)

f. Mshairi anasema kamwe hatoki kwake. Anaashiria chini ya mti waliozikwa babu zake na kusisitiza kwamba hawezi akaondoka (al. 3)

g. Inkisari – (i) Sendi – Siendi Nende wapi – Niende wapi

(ii) Kuboroga sarufi mf yangu mimi ni ardhi hii – Ardhi hii ni yangu mimi (1 x 1)

h. Karatasi – Hati miliki

Nimesaki – Nimebaki

Kitovu – Asili

(al. 3 x 1)

. . **SEHEMU B TAMTHILIA YA KIGOGO**

KIGOGO

2i) – Maneno ya Majoka

- Anamwambia Ashua
- Ofisini mwa Majoka
- Ni baada ya Ashua kumkataa Majoka Kimapenzi alipokwenda kutaka msaada kwake

1 x 4 = 4

ii) Mbinu – Swali la balagha – uliona nini kwa huyo zebe wako? (al 2)

- Nidaa – Eti mapenzi! (al 2)
- Kutaja alama 1
- Mfano alama 1

iii) Hulka za Majoka

- Dharau/ bezo – Eti mapenzi!
- Mpyaro – zebe (mjinga / mpumbavu) 1 x 2 = 2

1x 2 = 2 Mwalimu akadirie

iv) **Ukandamizaji wa mwanamke**

- kupigwa: Ashua akiwa gerezani anapigwa na askari
- kubezwa / kukejeliwa: Tunu anakejeliwa na Ngurumo na walevi wengine
- Chombo cha mapenzi. Majoka anamtaka Ashuakimapenzi anapokwenda kumwomba msaada.

- Kijakazi nyumbani. Majoka anamtuma chopi kumuagiza mkewe kumpikia kuku na nyama na kumuokea chapatti

- Kutusiwa. Boza anamwambia Sudi kuwa asifikiri kuwa yeye anauza nyong'a kama Tunu wake.

- <u>Kufungwa.</u> Ashua anafungwa na Majoka

- <u>Kunyimwa kura/uongozi.</u> Nurumo anamwambia Tunu kuwa kama hampi kura Majoka ni heri ampe paka wake. Majoka lakini si mwanamke Tunu.

- <u>Kunyimwa ajira.</u> Licha ya Ashua kufuzu taaluma ya ualimu, hakuajiriwa na serikali. Anaishia kuchuuza maembe sokoni la chapakazi.

- <u>Kuozwa bila hiari.</u> Majoka nataka kumwoza Tunu kwa mwanawe Ngao Junior bila hiari yake.

- <u>Kunyimwa fidia.</u> Majoka alitaka kumnyima Hashima fidia baada ya kifo cha mumewe

3.Tamaa ya kupata sanamu/ Majoka anataka Sudi amtengenezee sanA

- Tamaa ya kupata kodi. Majoka anawatoza kodi wafanyibiashara wa soko la Chapakazi kwa manufaa yao.

- Tamaa ya shule zao kufunzwa na walimu waliofuzu vyuoni. Majoka anamrai Ashua afunze katika shule zake.

- Tamaa ya **<u>kuungwa</u>**. Majoka anapata uungwaji mkono kupitia watu kama Ngurumo, Asiya na Boza -

- Anawapa hongo ili wamuunge mkono.

- Tamaa ya kupewa sifa lufufu. Kwa mfano Majoka lazima atangazwe katika vyombo vya habari.

- Tamaa ya kutafutia wanao wachumba. Majoka anamtaka Tunu aolewe na mwanawe Ngao Jur.

- Tamaa ya mapenzi - Majoka ana tamaa ya kupendwa na Ashua.

- Tamaa ya kujenga nyumba za kifahari. Majoka anatamani kujenga hoteli ya kifahari katika soko la Chapakazi.

- Tamaa ya **<u>usalama</u>** - Majoka ana walinzi wengi.

- Starehe na anasa. Majoka ana tamaa ya burudani. Anaenda kuogelea katika hoteli ya' Majoka and Majoka resort'

- Tamaa ya viongozi kurithisha jamaa zao uongozi.

Chozi la heri

4.Weka dondoo katika muktadha wake. (al.4)

i) Mzungumzaji ni Ridhaa

ii) Anayezungumziwa ni Kaizari

iii) Ni katika kambi/mabanda- Kwenye Msitu wa Mamba

iv) Ni baada ya Kaizari kumsimulia Ridhaa magumu aliyoyapitia kutoka kwake nyumbani hadi kujipata kweye hali nyingine ngumu katika kambi.

b) Ni hali gani inayorejelewa kwenye dondoo. (al.6)

i) Mke wa Kaizari, Subira ananyakwa kofi kubwa

ii) Anarejelewa kama kidume kijoga-kudharauliwa

iii) Mke wake anakatwa kwa sime na kuzirai kwa uchungu

iv) Bintize –Lime na Mwanaheri- wanafanyiwa unyama na mabarobaro

v) Jirani yake Tulia anamfukuza anapojaribu kuwapa mke wake na watoto huduma za kwanza

vi) Wanawe wanazirai ubavuni mwake

vii) Anaabiri gari bila kujua waendako na jamaa zake

viii) Walitazama mabasi yakichomwa kwenye safari iliyokuwa ndefu

ix) Gari linaisha petroli- wanajitoma msituni

x) Wanakula mate usiku wa kwanza kutokana na ugeni/ukosefu wa chakula

xi) Kuna hali mbaya ya baridi na umande wa asubuhi

xii) Wanakosa maji safi ya kunywa kwenye msitu

xiii) Kunywa maji ya Mto wa Mamba kunawasababishia homa ya tumbo.

xiv) Vijumba vichache havikutosha kuhimili idadi ya wakimbizi

xv) Huduma za kijamii zinaadimika –ukosefu wa misala na misala ya kupeperushwa

xvi) Sandarusi za kutumiwa kama misala zilitafutwa mbali kwenye milima ya taka.

xvii) Roho za watoto zilibwakurwa na magarimoshi kwenye reli walipoenda haja kule

xviii) Kuna hali ya njaa na vilio vya watoto wenye njaa

5. i. Subira alitengwa na familia ya mume wake kwa kuwa wa kabila tofauti na lao

ii. Mwanaheri anatueleza kuwa mama yake alikuwa ametoka kwenye jamii ya mamwezi lakini babake alikuwa wa jamii tofauti. Kila mara subira aliitwa ‘muki’ au huyo wa kuja

iii. Kijana mmoja alimwita Ridhaa mfuata mvua jambo lilimuumiza sana Ridhaa.

iv) Mzee kendi alimtendea udhalimu Ridhaa na kuiteketeza aila yake licha ya wao kuwa majirani kwa miaka hamsini. Ridhaa alifanyiwa hivi kwa kuwa alikuwa ametoka kwenye kabila tofauti na mzee kendi.

vi) Ndoa ya Selume ilisabaratika baada ya vita vya kutawazwa kwa kiongozi mpya.

kuoa msichana wa kikwao.

iii) Tulia alimsaidia kaizari kufunganya na kumsidikiza hadi njia panda. Alimkumbatia na kumwambia kuwa mwenyezi Mungu ndiye hupanga na nguvu na mamlaka pia hutoka kwake

ix) Uongozi mpya umezua uhasama kati ya koo ambazo zimeishi kwa amani kwa karibu karne moja.

x) Subira aliweza kuvumilia kubaguliwa, kufitiniwa na kulaumiwa kwa asiyoyatenda, Mwishowe alihiari kujiondokea na kwenda mjini alikojinywea kinywaji kikali. (zozote 10 x 2)

TUMBO LISILOSHIBA

6. a) <u>Mapenzi ya kifaurongo</u>

i) Ndoa iliyotarajiwa ya Dennis na Penina ilitawaliwa na unafiki. Penina anamjia Dennis na wazo la kuwa wapenzi bila kuzingatia hali duni ya familia yake. Dennis anapokosa ajira anamfukuza

ii) Inatawaliwa na kuhimiliana

iii) Imetawaliwa na kukata tamaa - Penina anakata tamaa baada ya Dennis kukosa kazi

iv) Imezingirwa na utabaka wa kiasili

v) Mapenzi hukua, huugua na hufa 5 x 1 = 5

Masharti ya kisasa

Ndoa ya Dadi na Kidawa

i) Ndoa inayodhibitiwa na masharti

ii) Ndoa ya kugawana majukumu

iii) Ndoa ya kupanga uzazi

iv) Ndoa inayoruhusu mwanamke kufanya kazi. Kidawa anafanya kazi ya umetroni usiku na kuuza bidhaa mtaani

v) Baadhi ya watu huingilia ndoa za wenzao kama njia ya kuona mapenzi yamevunjika baina ya wanandoa husika
5 x 1 = 5

Mtihani wa maisha

- wazazi wa Samueli ni wenye mapenzi wanaonyesha mapenzi kwa mtoto huyu wao kwa kumpeleka shuleni akajipatie elimu

- Samuel anaonyesha mapenzi kwa Nina. Kwa muda amekuwa mpenziwe

- Nina anaamini kuwa mwanaume huyu ni bingwa kutokana na kudanganywa alikodanganywa na mwanaume huyu

- mamake Samueli ana mapenzi ya dhati kwake, baada ya Samuel kujaribu kujitoa uhai mamake anamsihi waende nyumbani “Twende zetu nyumbani mwanangu.” zozote 4 x 1 = 4

Ndoto ya Mashaka

i) Kuna ndoa ya Mashaka na Waridi

ii) Kuna ndoa ya mtumwa na mumewe mzee Rubeya

iii) Tatizo la kwanza ni ndoa ya kulazimishwa. Mashaka na Waridi walitoka kwenye matabaka mawili tofauti

Waridi - tabaka la kitajiri

Mashaka - tabaka la maskini

v) Kuna kutohusisha wanawake katika ndoa. Mamake Waridi hakuhusishwa katika harusi

vi) Ndoa inakumbwa na tatizo la malazi bora - upendo, kujikubali, ukosefu wa taasubi ya kiume

vii) Kuna changamoto zinazojitokeza baada ya kifo cha mmoja. Mashaka anawachwa yatima

viii) Kuna utengano katika ndoa. Waridi anatengana na mumewe kutokana na hali ngumu ya kiuchumi

7. a) Maneno haya yanasemwa na Mbura

- alikuwa anazungumza na Sasa

- walikuwa kwenye sherehe iliyoandaliwa na mzee Mambo

- walikuwa wanazungumza kuhusu ‘kula kwao’ 4 x 1 = 4

b) <u>Sifa za Mbura</u>

- ni mzalendo - anafanya kazi kwa bidii katika wizara yake kama njia ya kuonyesha uzalendo

- mwenye tamaa - anajaza sahani kwa chakula na kukila chote

- mwenye utu - anataka wananchi wale kwa niaba ya viongozi kama vile wao wamekuwa wakila kwa niaba yao

- ni fisadi - amepokea kazi kwa afisi ya serikali kwa njia isiyo halali

- mzembe - baada ya kula sahani tatu za vyakula kwenye sherehe analala usingizi mzito badala ya kwenda kazini

- mtetezi wa haki - mvumilivu-

- mpyoro

- msema kweli zozote 6 x 1 = 6

c) <u>Jinsi viongozi walivyo wabadhirifu</u>

- hulipwa mishahara mikubwa sana na serikali jambo linalochangia ubadhirifu wa mali ya umma

- sherehe kubwa za viongozi wa kiserikali huchangia pakubwa ubadhirifu

- viongozi hutumia raslimali za nchi kwa manufaa yao ya kibinafsi - magari ya serikali

- raslimali zilizotumiwa katika kuvinunua vyakula na vinywaji vingetumika katika kuendeleza asasi tofauti za kijamii

- DJ na wenzake wanapata mabilioni ya fedha kutokana na kuwatumbuiza wageni katikasherehe kama hizi

- viongozi wanawachukua baadhi ya watu wao wa karibu na kufanya juu chini kuona kwamba wanajifaidi na mali na raslimali za wananchi pasipo kuzitolea jasho kamwe

- upeperushaji wa matangazo katika vyombo vya habari ya sherehe za kiongozi binafsi ni njia ya kuendeleza ubadhirifu wa raslimali za umma

- Mbura na Sasa wanaendeleza ubadhirifu pale wanapoamua kuchukua vyakula kupita kiasi katika sherehe za mzee Mambo

- kuwaajiri viongozi wawili wenye nyadhifa sawa katika sekta tofauti za umma

- vibaraka na vikaragosi kupewa mali ambayo ingewafaidi wananchi zozote 10 x 1 = 10

8: FASIHI SIMULIZI

1. a) Fafanua mchakato wa uwasilishaji wa vitendawili. (al.4)

    1. Kitangulizi- Mtegaji: kitendawili

    Mteguaji: tega

    2. Swali lenyewe- kitendawili kutegwa

    3. Majibu kutolewa

    4. Mtegaji asipooridhika huomba kupewa zawadi kisha hutoa jibu.

b) Linganisha na ulinganue vitendawili na methali. (al.10)

Mfanano

1. Zote ni tungo fupi za semi
2. Zote huwa na maana fiche
3. Zote hutumia lugha inayojenga taswira
4. Zote huwa na miundo maalum ya lugha

5. Zote hupata maana kulingana na jamii

Tofauti

1. Vitendawili vina fomyula ilhali methali hazina fomyula
2. Fumbo la kitendawili hufumbuliwa papo hapo fumbo si lazima kufumbuliwa papo katika methali.
3. Vitendawili hutumiwa na watoto sana, methali hutumiwa kuonyesha hekima miongoni mwa watu wazima na wazee
4. Vitendawili hutolewa katika vikao maalum, methali si lazima kutengewa vikao maalum.
5. Vitendawili hutumia lugha ya majibizano , methali aghalabu huwa kauli moja ya msemaji.
6. Hadhira tendi huwa katika vitendawili , katika methali hadhira si lazima iwe tendi.

C) Uhamaji wa watu huwafanya kuacha utamaduni wao.

- ✔ watu kuwa na mtazamo hasi kuhusu fasihi simulizi
- ✔ ubidhaaishaji wa fasihi simulizi- kuandika kitabu kama vile cha methali na kubadilisha umiliki
- ✔ watu kupendelea kusoma
- ✔ mwingiliano wa watu huwafanya kusahau fasihi yao
- ✔ teknolojia yasasa ambayo fasihi simulizi huhifadhiwa badala yaakilini.
- ✔ Utamaduni wa fasihi simulizi umebadilika – babu na bibi hawawatambii watoto hadithi. Mwalimu akadirie